

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO**

Simu: +25526-230081
Nukushi: +25526-2321170
Barua pepe: km@habari.go.tz
Tovuti: www.habari.go.tz



P.O. Box 25,
Mtaa wa Habari,
Mji wa Serikali Mtumba,
40481 Dodoma.

TAARIFA KWA UMMA

**KIKAO NA WABUNIFU WA MIFUMO YA KUUZA FILAMU, MUZIKI NA KAZI ZA
WABUNIFU KWA NJIA YA KIDIJITI**

Dodoma- Desemba 15, 2020

Katibu Mkuu Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo na Msemaji Mkuu wa Serikali Dkt. Hassan Abbasi anawaalika wabunifu wote wa Mifumo ya kuuza Filamu, Muziki na wabunifu kwa njia za Kidijiti, katika kikao cha kuonesha namna mifumo hiyo inavyofanya kazi kwa lengo la kusaidia kupatikana kwa namna bora itakayosaidia kusambaza kazi za wabunifu nchini.

Kikao hicho kitakuwa tarehe 17 Desemba, 2020, kuanzia saa nne kamili asubuhi (04:00 asubuhi) katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNICC), Ghorofa ya Tatu, Ukumbi wa Idara ya Habari Maelezo, Dar es Salaam. Uongozi wa wizara unaomba kila mwenye mfumo huo afike katika kikao hicho.

Aidha, kila mbunifu atapewa fursa ya peke yake kueleza namna mfumo wake unavyofanya kazi na atapewa kwa muda wa dakika 15 wa kufanya wasilisho.

Kwa mawasiliano zaidi piga simu Na. 0759 246 000.

Imetolewa na;

Eleuteri E. Mangi

**Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini
Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo**